



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UCHUKUZI

MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI



TAARIFA KWA UMMA

**KUSITISHWA KWA LESENI NA RATIBA ZA MABASI 35 YA KILIMANJARO  
TRUCK COMPANY LIMITED**

Kwa mujibu wa kifungu cha 5(1)(b) cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini, Sura ya 413, Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) ina jukumu la **kutoa, kuhuisha na kufuta vibali na leseni za usafirishaji**. Aidha, Kanuni za Leseni za Usafirishaji (Magari ya Abiria) za Mwaka 2020 (Tangazo la Serikali Na. 76 la tarehe 7/2/2020), inaelekeza watoa huduma za usafiri wa mabasi kutumia mfumo wa Tiketi Mtandao ulioidhinishwa na LATRA na pia kutoza nauli zilizoidhinishwa na LATRA.

Katika kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria, LATRA imekuwa ikichukua hatua na kukutana na uongozi wa *Kilimanjaro Truck Company Limited*, kutokana na kampuni hiyo kukiuka Sheria na Kanuni mara kwa mara. Ukiukwaji huo ni pamoja na kuzidisha ukomo wa nauli ulioidhinishwa na Mamlaka, kutotumia mfumo wa Tiketi Mtandao ulioidhinishwa na Mamlaka na kutoa huduma bila kuzingatia ratiba za safari.

Baada ya kujiridhisha kuwa mtoa huduma huyu ameendelea kukiuka Sheria, Taratibu na Kanuni kwa makusudi, hata baada ya kutembelewa, kushauriwa na kuelekezwa kwa barua, Mamlaka inautangazia umma kuwa **inasitisha leseni na ratiba za mabasi 35 ya *Kilimanjaro Truck Company Limited* kuanzia Jumatatu tarehe 8 Januari, 2024**. Kampuni hii itaruhusiwa kurejesha huduma za mabasi yake baada ya kuwa na mfumo wa Tiketi Mtandao, kuingiza nauli zisizozidi viwango vilivyoidhinishwa na LATRA kwenye mfumo huo, na kuwasilisha maombi yatakayoridhiwa na LATRA.

Mamlaka inawakumbusha watoa huduma wote kuwa kutotumia mfumo wa Tiketi Mtandao na kutoza abiria nauli zaidi ya viwango vilivyoidhinishwa na LATRA ni kosa kwa mujibu wa Sheria na Kanuni zilizopo. Watumia huduma (abiria) tupeni taarifa kwa simu ya bure (toll free) namba 0800 110019/20 wakati wowote, usiku na mchana (24/7).

Imetolewa na:

CPA Habibu J. S. Suluo

**MKURUGENZI MKUU**

06 Januari, 2024





JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UCHUKUZI

MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI



ORODHA YA MABASI 35 YA *KILIMANJARO TRUCK COMPANY LIMITED*  
YALIYOSITISHIWA LESENI KUENZIA TAREHE 8 JANUARI, 2024

Na	Namba ya Usajili	Njia (Route)	Leseni ya LATRA
1	T491ARB	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A4A214433
2	T165DMH	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A4A213378
3	T772ADJ	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A4A213017
4	T830AXR	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A4A213822
5	T676DHY	DAR ES SALAAM - NAMANGA	A4A213237
6	T805DDB	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A4A213277
7	T689DHY	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A4A212037
8	T893APD	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A4A214001
9	T814BGZ	DAR ES SALAAM - NAMANGA	A4A213494
10	T545BHY	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A4A212786
11	T639AQN	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A4A213992
12	T278ALQ	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A4A212248
13	T860BVA	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A3A290396
14	T708DGQ	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A4A213427
15	T163DMH	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A4A213389
16	T540AQK	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A4A213877
17	T675DHY	DAR ES SALAAM - NAMANGA	A4A213258
18	T705DGQ	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A4A211656
19	T855AXR	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A4A213854
20	T804DDB	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A4A211889
21	T895APD	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A4A213676
22	T709DGQ	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A4A213619
23	T622DPT	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A4A213021
24	T983AWY	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A4A214099
25	T904ACN	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A4A212137
26	T546BHY	DAR ES SALAAM - NAMANGA	A4A212365
27	T178EAU	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A4A213841
28	T176EAU	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A4A213856
29	T173EAU	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A4A213878
30	T177EAU	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A4A213866
31	T832ASM	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A4A213855
32	T434DKL	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A4A211949
33	T809BGZ	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A4A213846
34	T871BVA	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A3A289383
35	T706DGQ	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A4A213650